# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO

## GOVERNMENT e-PAYMENT GATEWAY (GePG)

### MAELEZO KUHUSU MFUMO WA GePG

**TOLEO LA FEBRUARI, 2022**

**YALIYOMO**

**1.0 UTANGULIZI** ..... 1
1.1 KUANZISHWA KWA GePG ..... 1
1.2 UKUSANYAJI WA FEDHA ZA UMMA KABLA YA GePG ..... 1
1.2.1 Changamoto katika ukusanyaji wa Fedha za Umma ..... 1
**2.0 MFUMO WA GEPG UNAVYOFANYA KAZI** ..... 2
2.1 FAIDA ZA KUANZISHWA KWA GePG ..... 3
2.1.1 Faida kwa Serikali Kuu ..... 3
2.1.2 Faida kwa Mabenki / Mitandao ya simu/Mawakala ..... 3
2.1.3 Faida kwa taasisi za Umma ..... 3
2.1.4 Faida kwa Mlipaji wa Huduma za Umma ..... 3
2.2 WADAU WALIOUNGANISHWA NA MFUMO WA GePG ..... 3
2.2.1 Taasisi za Umma ..... 3
2.2.2 Mabenki ..... 4
2.2.3 Mitandao ya Simu za Mkononi ..... 5
**3.0 MIFANO HAI YA FAIDA ZA GePG KWA TAASISI ZA UMMA.** ..... 5
**4.0 MAWASILIANO** ..... 6

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 KUANZISHWA KWA GePG

GePG ni kifupi cha "**Government e-Payment Gateway System". H**uu ni Mfumo wa kielektroniki unaowezesha ukusanyaji wa fedha za umma kielektroniki Serikalini. Mfumo huu umebuniwa na kutengenezwa na wataalamu wa ndani wa Serikali.

Mfumo wa GePG unasimamiwa na **Wizara ya Fedha na Mipango** kiufundi na kiundeshaji. Miundombinu ya mfumo huu imesimikwa kwenye kituo cha kuhifadhi DATA cha Serikali (Government Data Center) kinachosimamiwa na Wakala ya Serikali Mtandao(eGA). Aidha Mfumo huu upo kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma (PFA) ya mwaka 2001 kupitia marekebisho ya mwaka 2017 (Sura 348), na Waraka wa HAZINA Namba 3 wa mwaka 2017. Sheria ya Fedha za Umma inawataka Maafisa Masuuli wote kukusanya fedha za Umma kwa kupitia Mfumo wa GePG.

Lengo kubwa la kuanzishwa kwa GePG ni kutatua changamoto zilizopo kwenye Mfumo uliokuwepo kwa ukusanyanji wa Fedha za Umma ili kuongeza Uwazi na Udhibiti wa Fedha za Umma, Kuboresha na kurahisisha namna ya kulipia huduma za Umma na pia kupunguza gharama zinazoambatana na ukusanyaji wa Fedha za Umma.

### 1.2 UKUSANYAJI WA FEDHA ZA UMMA KABLA YA GePG

Ukusanyaji wa Fedha za umma (Hasa zile zitokanazo na kodi na zile zitokanazo na Malipo ya Huduma zitolewazo na Serikali) umekuwa ukifanywa na taasisi za umma ambazo kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma zimepewa jukumu la kuzikusanya Fedha hizo. Katika kuongeza ufanisi kwenye ukusanyaji wa Fedha hizi, kila taasisi ilikuwa inajiwekea mikakati ya makusudi ya kuhakikisha inaboresha namna inavyotoa Ankara na pia namna Ankara hizo zinavyowafikia wateja na zinavyolipiwa.

Mikakati hiyo ilikuwa ni pamoja na kuhakikisha uandaaji wa Ankara na Ulipiaji wake unafanyika kwa njia za kielektroniki ambazo ni pamoja na kutumia Mabenki, Mitandao ya simu za mkononi na Mawakala wa Malipo ("Aggregators and Agents"). Pamoja na jitihada na mikakati yote hiyo, zoezi hili lilifanywa na kila taasisi ya umma peke yake. Zoezi hili pia lilihusisha wadau wengine waliokuwa wanakusanya pesa kwa niaba ya taasisi za umma ambapo ilipelekea changamoto nyingi kujitokeza katika zoezi la ukusanyaji.

#### 1.2.1 Changamoto katika ukusanyaji wa Fedha za Umma

Ukusanyaji wa Fedha za Umma uliokuwa ukifanywa na taasisi za Umma katika kipindi ambapo GePG ilikuwa haijaanzishwa ulikubwa na Changamoto zifuatazo;

- Gharama kubwa za miamala inayohusu makusanyo ya Fedha za umma

- Utaratibu usio rafiki kwa Mlipaji wa huduma za Umma unaoanzia namna anavyopatiwa Ankara, namna anavyolipia Ankara yake, namna anavyothibitisha malipo, kupatiwa Risiti na Mpaka anavyopatiwa huduma.
- Machaguo machache ya njia za kulipia (Mabenki, Mitandao ya simu za mkononi au Mawakala) kwa sababu kuongeza machaguo kulikuwa kunaongeza gharama za ukusanyaji kwa taasisi.
- Ilipohitajika kufungamanisha Mfumo wa Ankara wa taasisi na Mifumo ya Ulipaji (kama vile mabenki, Mitandao ya simu za mkononi na Mawakala wakubwa (Aggregators) gharama ilikuwa kubwa kwa sababu kila Mfumo utafungamanishwa peke yake
- Ilikuwa ni vigumu sana kupata taarifa ya Makusanyo yanayofanyika kwa wakati huo huo ("Real time information")
- Taasisi kusimamia mikataba mingi inayohusu makusanyo ya Fedha za Umma kwa kuwa kila njia ya kulipia ilitakiwa kuwa na mkataba wake.
- Tofauti katika viwango ambavyo kila taasisi ilikuwa inalipia kama gharama ya miamala kwa njia moja ya Malipo (Kwa mfano; Benki / Mtandao mmoja wa Simu unakuwa unatoza viwango viwili tofauti kwa taasisi mbili za Umma anazozikusanyia Fedha za Umma)
- Fedha zinazokusanywa na taasisi ya fedha kutoingia moja kwa moja kwenye account ya taasisi inayotoa huduma mpaka baada ya kipindi fulani ili kurusu usuluhishi (Reconcilliation) wa miamala kufanyika kwanza.

## 2.0 MFUMO WA GEPG UNAVYOFANYA KAZI

Mfumo wa GePG umefungamanishwa(integrated) na Mifumo ya kielektroniki ya taasisi za Serikali ambayo huwezesha malipo kwa kutoa Ankara Pepe (electronic bills/Invoices). Kwa taasisi ambazo kwa sasa hazina Mfumo wa kielektroniki wa kutolea Ankara Pepe (Billing System), GePG inawapatia Mfumo kwa ajili ya kuandalia Ankala Pepe (Generic Billing Portal).

Aidha mfumo huu pia umeunganishwa kielektroniki na Mifumo ya kielektroniki ya taasisi zinazotoa huduma za Ulipiaji kama vile Mabenki na Makampuni ya Mitandao ya Simu za Mikononi kwa kupitia Makampuni yao tanzu ambayo hutoa huduma za kifedha kwa kibali cha Benki Kuu ya Tanzania.

Hivyo mfumo wa GePG una uwezo wa kutoa namba ya malipo ("Control number") kwenye Ankara Pepe (electronic bill/invoice) kwa kila malipo yanayofanyika na kisha Walipiaji wa huduma hutumia namba hizo kulipia huduma kwenye makampuni yanayotoa huduma za Ulipiaji.Baada ya malipo kufanyika GePG hutoa stakabadhi ya kielektroniki (electronic Exchequer Receipt Voucher – e-ERV) ambayo huituma kwa njia ya ujumbe mfupi (sms) kwa mlipaji na pia kwenye Mfumo wa taasisi iliyotengeneza Ankara hiyo. Taarifa zote za Malipo hutunzwa kwenye kanzidata ya mfumo wa GePG kadri malipo husika yanavyofanyika.

Kwa Kupitia Mfumo huu, Wizara, Idara, Wakala na Taasisi zote za Umma wanaweza kukusanya Fedha za Umma kwa njia mbalimbali za kielektroniki ikiwemo Mabenki na Mitandao ya simu iliyounganishwa na GePG. Mpaka sasa, mitandao yote sita (6) ya simu imeshaunganishwa.

## 2.1 FAIDA ZA KUANZISHWA KWA GePG

Mfumo wa GePG umeleta faida na tija kubwa katika ukusanyaji wa Fedha za Umma. Kila mdau katika zoezi la ukusanyaji wa Fedha za Umma amenufaika na Mfumo huu kwa namna zifuatazo;

### 2.1.1 Faida kwa Serikali Kuu

- Kuongezeka kwa Uwazi na Udhibiti katika Ukusanyaji wa Fedha za Umma
- Kupata taarifa sahihi na kwa wakati zinazohusu makusanyo
- Kuwa na Viwango na utaratibu unaofanana katika ukusanyaji wa Fedha za Umma kwa taasisi zote za Umma
- Kuchochea ubunifu katika ukusanyaji wa pesa za Serikali na sekta ya Fedha kwa ujumla kwa kuweka mazingira rafiki na ya usawa kwa Wakusanyaji
- Kutoa huduma bora na rahisi ya Malipo ya Fedha za Umma hivyo kuchochea ongezeko la makusanyo
- Fedha kufika haraka katika akaunti kuu za Makusanyo zilizoke benki kuu.

### 2.1.2 Faida kwa Mabenki / Mitandao ya simu/Mawakala

- Sehemu moja tu ya kuunganisha mifumo yao na Mifumo wa taasisi za Umma ("Single point of Linkage"), hivyo kuzifikia taasisi za umma na kutoa hudum za kifedha kwa urahisi.
- Mazingira rafiki na ya Usawa katika Ukusanyaji wa Fedha za Umma

### 2.1.3 Faida kwa taasisi za Umma

- Kupunguza gharama zitokanazo na uwekezaji katika miundombinu ya Tehama pamoja na "Software Development" katika suala la ukusanyaji wa mapato
- Urahisi katika usuluhishi wa Miamala na Usuluhishi wa taarifa za kibenki
- Kupata taarifa sahihi na kwa wakati zinazohusu makusanyo
- Kupunguza gharama za miamala inayohusu ukusanyaji wa Fedha za Umma.

### 2.1.4 Faida kwa Mlipaji wa Huduma za Umma

- Machaguo mengi ya njia za kulipia huduma za Umma (Benki, Mawakala wa Benki, na Mitandao ya simu).
- Urahisi wa kulipia huduma za Umma na hivyo kuokoa muda.

## 2.2 WADAU WALIOUNGANISHWA NA MFUMO WA GePG

### 2.2.1 Taasisi za Umma

Watoa Huduma/Taasisimbalimbali za umma zimeendelea kuunganishwa na GePG ili kukidhi matakwa ya sheria ya Fedha za Umma. Mpaka tarehe 28 Februari 2022 , idadi ya watoa huduma /taasisi zilizounganishwa na kutumia Mfumo kukusanya Fedha za Umma ni mia saba arobaini na tatu (743). Taasisi zilizounganishwa ni pamoja na;

- Halmashauri zote nchini (185)
- Hospitali
- Wizara na Idara za Serikali
- Mashirika na Taasisi za Umma, n.k.

### 2.2.2 Mabenki

Benki mbalimbali zilizokidhi vigezo zimeshaunganishwa na GePG na zinasaidia ukusanyaji wa fedha za umma kwa kutumia namba ya Malipo (Control number) kutoka kwenye mfumo. Kufikia 28 Februari 2022 jumla ya benk 28 zimejiunga ambazo ni;

| Na. | Jina la Benki |
|---|---|
| 1. | ABSA BANK TANZANIA LIMITED |
| 2. | Akiba Commercial Bank |
| 3. | AMANA BANK |
| 4. | AZANIA Bank |
| 5. | BARODA BANK |
| 6. | Bank of Africa |
| 7. | BANK OF TANZANIA |
| 8. | CANARA BANK |
| 9. | NCBA |
| 10. | CITI BANK |
| 11. | CRDB Bank |
| 12. | DCB Commercial Bank |
| 13. | DIamond Trust Bank |
| 14. | ECOBANK |
| 15. | EQUITY BANK |
| 16. | EXIM |
| 17. | Guaranty Trust Bank |
| 18. | Habib Group Bank |
| 19. | I&M Bank (T) ltd |
| 20. | KCB BANK |
| 21. | National Bank of Commerce |
| 22. | National Microfinance Bank |
| 23. | Peoples Bank of Zanzibar |
| 24. | Standard Chartered Bank |
| 25. | Stanbic Bank |
| 26. | Tanzania Investment Bank Corporate Bank Ltd |
| 27. | Tanzania Postal Bank |
| 28. | UNITED BANK OF AFRICA |

### 2.2.3 Mitandao ya Simu za Mkononi

Kuna Mitandao ya Simu mbalimbali ambayo imeunganishwa na GePG na inatumika kukusanya Fedha za Umma. Mitandao ya simu za mkononi ambayo imeunganishwa kufikia 20 Februari 2022 ni pamoja na:

- T – Pesa (TTCL)
- M- Pesa (Vodacom)
- TigoPesa (Tigo)
- Hallopesa (Hallotel)
- Airtel Money (Airtel)
- Ezy Pesa (Zantel)

## 3.0 MIFANO HAI YA FAIDA ZA GePG KWA TAASISI ZA UMMA.

Takwimu zinaonesha kuwa mapato ya baadhi ya Taasisi za Umma yamengozeka kwa kipindi cha mwaka mmoja (1) kutoka 2016/17 mpaka 2017/18 baada ya taasisi hizo kujiunga na mfumo wa GePG. Baadhi ya Taasisi hizo zimeokoa gharama kubwa zilizokuwa zinatumika kuwalipa wazabuni wa mifumo ya ukusanyaji wa fedha za Umma. Pia Taasisi nyingine zimeweza kuboresha huduma hasa katika eneo la ulipaji wa huduma za serikali. Mfano wa Taasisi hizo ni:

1. Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO) ilikuwa ikilipa zaidi shilingi bilioni 38 kwa Mwaka, kwa mawakala wa kuuza umeme. Baada ya kufunga mfumo wa GePG kwa sasa shirika halilipi chochote.

2. Wakala wa Vipimo (WMA) walikuwa wakikusanya wastani wa shilingi bilioni 1.0 kwa mwezi, baada ya kujiunga na Mfumo wa GePG inakusanya wastani wa zaidi ya shilingi bilioni 2.5 kwa mwezi.

3. Mapato ya Wizara ya Ardhi yameongezeka kutoka shilling bilioni 70 mpaka Zaidi ya shilingi bilioni 100.

4. Mapato ya Wizara ya Kazi, Ajira, Vijana, Wazee na Wenye Ulemavu yameongezeka kutoka kiasi cha shilingi bilioni 2.4 (kwa kipindi cha Julai mpaka Septemba, 2017) hadi kufikia kiasi cha shilingi bilioni 2.7 kwa kipindi kama hicho (Julai mpaka Septemba, 2018) baada ya kujiunga na GePG.

5. Mapato ya Wakala wa huduma za Misitu (TFS) yameongezeka kutoka shilingi bilioni 95 mpaka Zaidi ya shilingi bilioni 115.

**4.0 MAWASILIANO**

Katibu Mkuu,

Wizara ya Fedha na Mipango,

Mji wa Serikali – Mtumba,
Mtaa wa Hazina,
Sanduku la Barua 2802,
40468 DODOMA,
TANZANIA.

Dawati la Msaada: +255787 626 502 au +255 714 927 494
Call Center: +255 26 2160000

Barua pepe: gepg.support@hazina.go.tz

Tovuti: www.gepg.go.tz